**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**MAJARIBIO TOKA SEHEMU ZOTE TANZANIA**
**JARIBIO LA KWANZA JANUARI 2022**
**SOMO: URAIA NA MAADILI DARASA: VII**

**SEHEMU A: <u>CHAGUA HERUFI YA JIBU SAHIHI:</u>**

1. Viashiria vya Utandawazi ni pamoja na ……………
(A) kupungua kwa tofauti ya kipato (B) uchumi wa soko huria
(C) kupungua kwa umaskini (D) kuwepo kwa ushindani wa kutengeneza silaha
(E ) kuwepo kwa bidhaa nyingi toka viwanda vya ndani
2. Mojawapo ya njia ambazo wananchi wanaweza kushiriki katika ulinzi na usalama ni ………… (A) kupiga wahalifu (B) kufanya mazoezi ya viungo (C) kuwaua wahalifu (D) kuwafichua wahalifu (E ) kuwa rafiki na wahalifu
3. Moja wa matukio yanayokiuka Haki za Binadamu nchini Tanzania ni…...
(A) Mauaji ya vikongwe na maalbino (B) Ukataji na upandaji mid
(C) kuwafungulia mashataka wahalifu
(D) kufukuzwa kazi viogozi wasio waadilifu (E)Serikali kusimamia uksanyaji kodi
4. Zipi kati ya nchi zifuatazo ni wanachama wa Jumuiya ya Madola? ……
(A) Botswana na Burundi (B) Botswana na Zambia
(C) Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (D) Malawi na Burundi
(E ) Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
5. Matumizi ya Ofisi ya Umma kwa manufaa binafsi huitwa ……………….
(A) takrima (B) rushwa (C) uzalendo (D) ubinafsi (E ) ujasiriamali
6. Tofauti kati ya mila na desturi ni …………..……………….
(A) Mila hubadilika mara kwa mara kuliko desturi
(B) Desturi hubadilika mara kwa mara kuliko mila
(C) Mila ni mazoea wakati desturi ni vitendo
(D) Mila ni mazoea na huweza kubadilika na kuwa desturi
(E) Desturi hubadilika mara kwa mara kuliko mazoea
7. Wajibu wa serikali katika kujenga maadili ya viongozi ni …………….
(A) Kuwakopesha magari viongozi wote
(B) Kuimarisha mfumo wa chama kimoja cha siasa
(C) Kusimamia sheria za utumishi wa Umma
(D) Kuhamisha watumisha wasio waadilifu
(E ) Kuajiri watumishi wenye elimu ya juu tu
8. Maliasili zinazovutia watalii na kuchangia katika kukuza uchumi wa Tanzania ni............. (A) ardhi (B) mito (C) mifugo (D) madini
(E) mbuga za wanyama
9. Ipi kati ya sarafu zifuatazo ina picha ya Rais wa kwanza wa Zanzibar ? …
(A) Sarafu ya shilingi mia moja (B) sarafu ya shilingi mia mbili
(C) Sarafu ya shilingi hamsini (D) Sarafu ya shilingi ishirini
(E ) Sarafu ya shilingi kumi
10. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya huchanguliwa na ………………
(A) Mkurugenzi mtendaji wa Wilaya (B) Baraza la Madiwani (C) Waziri katika Ofisi ya Rais Afisa Mtendaji wa Kata (E) Wenyeviti wa vijiji
11. Chombo cha juu katika maamuzi kwenye serikali ya kijiji ni …………….
(A) Serikali ya kijiji (B) Kamati ya ulinzi na usalama (C) Mkutano Mkuu wa kijiji
(D) Afisa Mtendaji wa kijiji (E) Kamati ya Maendeleo ya kijiji
12. Mtu anayedhibiti mwenendo wa wanafunzi shuleni ni. …………....
(A) Mwenyekiti wa kamati ya shule (B) Mwalimu wa nidhamu (C) Mwalimu mkuu msaidizi (D) Mwalimu wa taaluma (E) Mwalimu wa somo
13. Nchi ambayo kwa sasa inaongozwa na Rais mwanamke baada ya aliyekuwa Rais kufariki_______
(A) Rwanda (B) Kenya (C) Tanzania (D) Msumbiji (E) Zambia
14. Mwenyekiti wa kikao cha maendeleo katika Kata ni ………
(A) Diwani wa Kata (B) Afisa Huduma za ugani (C) Afisa Maendeleo wa Kata
(D) Mratibu Elimu wa Kata (E ) Afisa Mtendaji wa Kata
15. Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa kwa pamoja zipo chini ya ……..
(A) Bunge la Tanzania (B) Serikali ya Mtaa (C) Serikali Kuu
(D) Wabunge wa kuchaguliwa (E ) Chama Tawala
16. Jukumu la kutunga sheria ndogondogo katika Halmashauri ya Wilaya ni la …
(A) Mkuu wa Wilaya (B) Afisa Sheria na Usalama wa Wilaya (C) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (D)Baraza la Madiwani (E) Wabunge wa Wilaya husika
17. Katika Nembo ya Taifa alama inayowakilisha maliasili ya Taifa ni…….
(A) mlima Kilimanjaro (B) mkuki (C) karafuu (D) pembe za ndovu
(E) mawimbi ya bahari
18. Ni muhimu kwa wapiga kura wenye sifa kushiriki katika uchaguzi wa Rais na Wabunge kwa sababu …………..
(A) ni njia ya amani ya kubadili uongozi wa nchi
(B) ni njia pekee ya kuimarisha utandawazi
(C) ni kanuni ya kuimarisha mshikamano
(D) ni kanuni ya mfumo wa vyama vingi (E
) ni njia pekee a kuleta mabadiliko ya katiba ya nchi
19. Kuzingatia sheria, haki za binadamu, ukweli na uwazi, na uhuru wa vyombo vya habari ni misingi ya (A) Urasimu (B) Utawala wa sheria (C) Ujamaawa kiafrika (D) Demokrasia ya Uwakilishi (E ) Utawala bora
20. Ipi kati ya orodha zifuatazo inawakilisha makundi ya kutetea haki za wanawake ?
(A) UWT, TAWLA na TAMWA. (B) TAMWA, TGNP na TAWALA.
(C) MEWATA, TGNP na TAWLA (D) UWT, TGNP na TAMWA.
(E) MEWATA, TGNP na UWT.
21. Jukumu la kuwalinda raia wa Tanzania na mali zao lipo mikononi mwa
(A) Jeshi la Wananchi la Tanzania (B) Idara ya Usalama wa Taifa
(C) Jeshi la Magereza (D) Jeshi la Mgambo (E ) Jeshi la Polisi
22. Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lilianzishwa mwaka
(A) 1961 (B) 1962 (C) 1964 (D) 1963 (E ) 1965
23. Ni muhimu kwa Tanzania kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa sababuni lugha
(A) inayozungumzwa na watu wengi Afrika Mashariki

(B) ya mawasiliano katika Umoja wa Mataifa (C) ya kufundishia shuleni
(D) inayounganisha Watanzania
(E ) ya mawasiliano katika Bunge la Tanzania

24. Zipo aina tatu za mipango ya uchumi ambayo ni mipango ya……………
(A) miaka kumi, kumi na tano na ishirini na tano (B) Taifa, Mkoa na Wilaya
(C) kilimo, biashara na viwanda (D) muda mrefu, dharura na muda mfupi
(E ) muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu

25. Moja ya athari mbaya ya utandawazi kwa Tanzania ni …………
(A) kuongezeka kwa idadi ya wageni nchini
(B) kumomonyoka kwa maadili katika jamii (C) kuongezeka kwa uhasama baina ya vyama vya siasa (D) kuongezeka kwa uhuru wa vyombo vya habari
(E ) ongezeko la matumizi ya teknolojia ya habari

26. Utawala wa sheria maana yake ni …………..
(A) wananchi kujichukulia sheria mkononi
(B) polisi kuadhibu wanaovunja sheria (C) sheria kuchukua mkondo wake
(D) mahakama kukamata wanaovunja sheria
(E ) mamlaka ya mahakama kutunga sheria

27. Jaji Mkuu wa Tanzania huteuliwa na: (A) Bunge (B)Waziri Mkuu
(C) Rais (D) Makamu wa Rais (E) mwanasheria Mkuu

28. Mojawapo ya udhaifu wa Umoja wa Mataifa ni:…………………
(A) kushindwa kuzuia kuenea kwa Utandawazi (B) Waafrika hawajawahi kupata nafasi katika uongozi wa juu katika Umoja wa Mataifa (C) baadhi ya watu tu ndio wenye kura ya turufu (D) kushindwa kupitisha maazimio ya haki za binadamu
(E ) kutokushirikishwa kwa Waafrika katika vikao vya baraza la usalama

29. Nini maana ya ujasiriamali?
(A) Biashara yoyote yenye faida (B) Uwekezaji kwenye biashara (C) Biashara ndogondogo (D) Sekta binafsi (E ) Ujasiri wa kumiliki mali

30. Utandawazi ni mfumo unaohamasisha:………………………………..
(A) teknolojia ya habari na mawasiliano katika nchi zinazoendelea
(B) haki sawa kwa kila mmoja duniani
(C) mfumo wa vyama vingi katika nchi zinazoendelea
(D) biashara huria baina ya mataifa
(E ) sekta binafsi katika nchi zinazoendelea

31. Mojawapo ya kazi za Mgambo ni: ………………..
(A) kukamata wahalifu na kuwapeleka kwenye kituo cha polisi
(B) kuadhibu wanaovunja sheria mijini (C) kuzuia ajali za moto (D) kukusanya kodi ya maendeleo mijini (E) kuzuia na kupambana na rushwa

32. Ulinzi na Usalama wa taifa letu ni jukumu la:
(A) Jeshi la Wananchi wa Tanzania (B) kitengo cha Usalama wa Taifa (C) Jeshi la Polisi (D) Mgambo (E ) kila mwananchi

33. Haki ya kumiliki mali iko katika kipengele kipi cha haki za banadamu?
(A) Kijamii na kiuchumi (B) Kisiasa na kiuchumi (C) Kikatiba na kisiasa (D) Kijamii na kisiasa (E ) Kijamii na Kiutamaduni

34. Chombo chenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani Tanzania ni: ……..
(A) Jeshi la Polisi (B) Tume ya Taifa ya chaguzi (C) Mahakama Kuu (D) Ofisi ya msajili wa vyama vya siasa (E ) Ofisi ya Waziri Mkuu

35. Sababu kubwa ya kuruhusu mfumo wa vyama vingi Tanzania ni: ………
(A) kutekeleza matakwa ya wahisani (B) kulinda haki za makundi maalumu katika jamii (C) kuvutia wawekezaji wa nje (D) kutekeleza maelekezo ya Umoja wa Mataifa (E ) kupanua demokrasia

36. Ngao ya Taifa inawakilisha: (A) umoja, uhuru, uwezo na mamlaka ya Taifa
(B) uhuru, umoja na rasilimali za Taifa (C) uwezo, uhuru, uoto wa asili na mamlaka ya Taifa (D) uhuru, umoja na mamlaka ya Taifa (E ) uhuru na umoja

37. Rangi nyeusi katika Bendera yetu huwakilisha: …………………
(A) Mimea (B) Madini (C) Watu (D) Ardhi (E ) Mbuga za wanyama

38. Katika muundo wa kiutawala wa serikali za mitaa,Wilaya na manispaa zinaongozwa na:…….. (A) Chama tawala (B) Mkurugenzi mtendaji
(C) Mkuu wa Wilaya (D) Kamati yenyewe (E) Afisa utawala wa Wilaya

39. Vyanzo vya mapato ya serikali za mitani pamoja na: …………………
(A) kodi ya kichwa na kodi ya rasilimali
(B) ruzuku, kodi na michango mingine
(C) kodi ya ardhi, na kodi ya rasilimali
(D) tozo katika mazao ya mali asili (E ) tozo za leseni za biashara

40. Kazi ya kamati ya shule ni: (A) Kusimamia maendeleo ya taaluma
(B) Kutoa ushauri juu ya maambukizi ya UKIMWI
(C) Kuidhinisha uteuzi wa waalimu (D) Kusimamia nidhamu ya waalimu
(E ) Kusimamia ujenzi na maendeleoya shule

**SEHEMU B: JAZA SEHEMU ZILIZOACHWA WAZI**

41. Spika wa bunge la jamhuri ya muungano wa Tanzania huchaguliwa na
_______________________________

42. _________________________ni mfumo wa Uongozi unaofuata misingi ya haki na sheria.

43. Taja nguzo tatu za Dola
(i) ___________________________________________
(ii) ___________________________________________
(iii) ___________________________________________

44. Ni ishara gani inayoonesha kwamba Taifa limepatwa na msiba mkubwa wa kitaifa _______________________________________________

45. Mwenye mamlaka ya kufanya uteuzi wa mabalozi wa kuwasilisha Tanzania nchi za nje _______________________________________________

**MAJIBU**

**1.** E

**2.** D
**3.** A
**4.** C
**5.** B
**6.** D
**7.** C
**8.** E
**9.** A
**10.** B
**11.** D
**12.** B
**13.** C
**14.** E
**15.** C
**16.** A
**17.** A
**18.** A
19. E
20. A
21. E
22. A
23. D
24. D
25. E
26. E
27. C
28. E
29. C
30. A
31. A
32. A
33. A
34. B
35. E
36. D
37. D
38. B
39. B
40. E
41. WABUNGE
42. UTAWALA BORA
43. (i) SERIKALI (ii) BUNGE (iii) MAHAKAMA
44. BENDERA YA TAIFA KUSHUSHWA NUSU MLINGOTI
45. RAIS